***BAADHI YA VIGEZO VYA KUONGOZA MAJAJI KUPATA WASHINDI***

## 1. FILAMU BORA YA MWAKA

Best film of the year

Filamu bora ya mwaka itaangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Mtiririko wa hadithi na Muswada husika
b. Upigaji picha (Angle & Shots)
c. Uigizaji wa kuuvaa uhusika kwa waigizaji wote
d. Mandhari
e. Mwangaza
f. Sauti
g. Muziki wa kusindikizia filamu (Background Music)
h. Ubunifu ama uvaaji wa mavazi yanayoendana na mandhari ya hadithi husika

### Ufafanuzi

**Hadithi nzuri na mpangilio bora wa matukio**
Jinsi hadithi Inavyoteka hadhira Na pia ina mpangilio mzuri katika utekelezaji wake

**Kuelimisha kujenga ufahamu**
Jinsi filamu inavyowapa hadhira kitu cha kuikiri kutafakari au kuchambua, inawaelimisha na kuwapa ufahamu katika mambo Kama ya kijamii, kisiasa na kiuchumi

**Mazingira**
Jinsi mazingira yanavyowiana na maudhui ya filamu

**Maono**
Jinsi filamu inavyotengeneza maono na kuibua hisia zenye kuleta uhalisia wa kweli

**Uigizaji mzuri wa mhusika mkuu na wahusika wote**
Jinsi muhusika mkuu na waigizaji wote walivyofanikiwa kuwavutia hadhira kwa uigizaji wao mzuri

**Sinematografia nzuri na ya kuvutia**
Namna ubora wa filamu unavyoonekana hasa katika kazi ya kamera Kama mwanga, uchukuaji wa picha, rangi na Pembe

**Matumizi bora ya muziki na sauti**
Ni jinsi gani muziki na sauti zinaendana na mwelekeo wa filamu na kuongeza mwelekeo mzuri

Hisia, uhalisia, upekee na ubunifu

## 2. WAIGIZAJI

**MUIGIZAJI BORA KIONGOZI WA KIUME**
Best Actor in a Leading Role
**MUIGIZAJI BORA KIONGOZI WA KIKE**

Best Actress in a Leading Role

**MUIGIZAJI BORA MSAIDIZI WA KIUME**

Best Actor in a Supporting Role

**MUIGIZAJI BORA MSAIDIZI WA KIKE**

Best Actress in a Supporting Role

**MUIGIZAJI BORA CHIPUKIZI WA KIKE**

Best up Coming Actress

**MUIGIZAJI BORA CHIPUKIZI WA KIUME**

Best up Coming Actor

**MCHEKESHAJI BORA**
Best Comedian

Kwa vipengele vya waigizaji wote sifa za kuwapata washindi zinafanana kama ifuatavyo:-

a. Kuuvaa uhusika wa vipande (Scenes) anazocheza katika filamu husika
b. Utamkaji wa maneno ( Dialog )
c. Muonekano wa Sura (Facial Expression) kutokana na matukio ya vipande husika
d. Uelekeo wa mwili (Movements) kutokana na vipande husika

**Ufafanuzi**

**Ushawishi**
Jinsi muigizaji alivyoweza kuteka hisia za hadhira kwa umahiri wake na Kufanya filamu iwe ya kuvutia kwa hadhira

**Kujiamini**
Ni jinsi gani muigizaji anajiamini ndani ya filamu na hata akiwa kwenye jamii yake kiasi cha kuweza Hadhira

**Ufahamu**
Jinsi muigizaji alivyo na ufahamu wa Tabia za binadamu, kiasi cha

kuweza kuweka ufanisi wa Kufanikisha hisia katika mvuto na matendo ya mtu

**Ubunifu na kutumia akili**
Uwezo wa kuwa mbunifu Katika uigizaji na kutumia akili na ikibidi katika uigizaji wake , kiasi cha kumfanya awe wa kipekee na mbinu zipi anatumia katika uigizaji wake na Kufanikiwa kumtengeneza muhusika wa pekee katika maisha halisi

## 3. MPIGA PICHA BORA (Sinematografia)

Best Cinematographer

Mpiga picha bora wa Filamu ataangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Ubora wa picha alizopiga
   - Upigaji picha (Angle & Shots)
   - Mwangaza
   - Muonekano wa picha inayozungumza

**Ufafanuzi**
**Ubunifu wa Pembe Na shoti**
Ni kwa jinsi gani mpiga picha amekuwa na jicho la ubunifu wa kisanaa, kiasi cha kuweza kutengeneza "shorts" na Pembe za picha ambazo zinaleta uhalisia na kuvuta hisia za hadhira.

**Mwanga**
Ni kwa jinsi gani mpiga picha ameweza kutengeneza mwanga katika picha ambao unagusa hisia za hadhira na unamtangeneza muhusika, mazingira na Kufanya filamu ivutie

**Lenzi**
Ni kwa jinsi gani mpiga picha ameweza kutumia lenzi kuteka hisia za hadhira, na jinsi mwendokasi wa filamu ulivyoleta uhalisia

## 4. MHARIRI BORA WA FILAMU

Best Film Editor

Mhariri bora wa Filamu ataangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Uungaji wa picha
b. Upangaji wa picha
c. Usikivu wa sauti

d. Rangi (Colour Correction)

## 5. MUONGOZAJI BORA WA FILAMU

Best Film Director

Muongozaji bora wa Filamu ataangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Upigaji picha (Angle & Shots)
b. Uigizaji wa kuuvaa uhusika kwa waigizaji wote
c. Mandhari
d. Mwangaza
e. Uvaaji wa mavazi yanayoendana na mandhari ya hadithi husika

Ufafanuzi

**Uongozaji wa wahusika**

Uwezo wa muongozaji kumuongoza muhusika na kumfanya ateke hisia za hadhira kwa kuleta uhalisia ndani ya filamu

**Uchaguzi wa mazingira**
Uwezo wa muongozaji kuchagua mazingira yanayoendana na maudhui ya filamu

**Ubunifu wa sinematografia**
Uwezo wa muongozaji kumuongoza sinematografa apige picha zinazoendana na maudhui na kuleta hisia za kweli kwa hadhira

**Ubunifu na mpangilio wa matukio katika picha**
Uwezo wa muongozaji kubuni matukio yenye hisia na kuyapanga katika Hali itakayoteka hisia za hadhira

## 6. MPAMBAJI BORA

Best Makeup Artist

Mpambaji bora wa Filamu ataangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Utengezaji wa viambatisho (Damu, vidonda n.k)
b. Utengenezaji wa Muonekano ( Uzee, Wendawazimu, Ugonjwa, n.k)

**7.**

VISUAL EFFECTS

Visual Effects itaangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Uhalisia wa Muonekano wa matukio yaliyotengenezwa
b. Muingiliano wa matukio na muswada husika

**Ufafanuzi**

**Ubunifu wa shoti na Pembe za picha**
Jinsi “shoti” za picha zilivyobuniwa kiasi cha kubadili muonekano wa filamu na kuleta uhalisia na kuweza kuiteka hadhira

**Ubunifu wa mazingira**
Jinsi mazingira yalivyobuniwa na kubadilishwa Kiasi cha kuendana na Hali ya filamu sambamba na maudhui ya eneo Hilo

**Ubunifu wa wahusika na viumbe**
Jinsi wahusika au viumbe vilivyotengenezwa ndani ya filamu Kiasi cha kuteka mawazo na hisia za hadhira

**Ubunifu wa vitu**
Kuongeza kitu, vitu au kuondoa kitu ndani ya filamu katika namna ambayo italeta hisia na uhalisia kwa watazamaji

**Mabadiliko maalumu ya mwendokasi**
Kubadili mwendokasi wa muhusika, kitu au kiumbe katika matendo yao, Kuongeza au kupunguza mwendokasi wao au mwendokasi wa sauti na mwanga Na Kufanya filamu iwe ya kuvutia zaidi kwa watazamaji

**Kufunika mapungufu madogo dogo**
Kuweza kufunika mapungufu madogo Kama kuongeza Mabadiliko ya jicho, kutoa wigi, nywere, kubadili rangi ya ngozi, mavazi na sauti kiasi cha kuvuta hisia za watazamaji

## 14. MUSWADA BORA WA KUNAKILIWA

Best Adapted Screenplay

Muandishi wa Muswada bora wa kunakiliwa atapatikana kwa kuwasilisha muswada wake na hadithi aliyonakili na vitaangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Maneno / Mazungumzo (Dialogue)

b. Upigwaji wa Picha (Shots)
c. Uigizaji / Vitendo (Actions)
d. Uhamaji (Transition)
e. Muingiliano kati ya hadithi na muswada
f. Usisimuaji (Suspense)

**Ufafanuzi**

**Mazungumzo**

Ni kwa jinsi gani mazungumzo baina ya wahusika yanaendana na mawazo yao, hisia na ushawishi, na yameweza kuonyesha uhusiano baina ya wahusika na kuwakilisha mtazamo wa uhalisia ndani ya mswada kama yalivyonakiliwa kutoka katika hadithi mama

**Mpangilio**

Ni kwa jinsi gani mwandishi amepangilia matukio makubwa ndani ya mswada, hasa kunapokuwa na matendo makubwa, pia na muda uliotumika kuruhusu matukio hayo

**migogoro**

Ni kwa kiasi gani mwandishi amefanikiwa kutengeneza migogoro iliozalisha Maigizo, iliyotengeneza vikwazo,hisia na ushawishi kiasi cha kuteka akili za hadhira , pia migogoro iliyopangiliwa vizuri na kuleta uhalisia

**Wahusika**

Ni jinsi gani wahusika wameshabiina na matukio na vikwazo ndani ya hadithi, na kiasi walichofanikiwa kuendesha matukio kupitia hisia zao,matendo Yao na utashi wao kiasi cha Kufanya hadhira ahisi Kama wao hata Kama matukio hayo sio ya kweli

## 15. MUSWADA BORA HALISIA

Best Screenplay

Muandishi wa Muswada bora atapatika kwa kuwasilisha muswada halisi husika na katika muswada wake vitaangaliwa vitu vifuatavyo:-

g. Maneno / Mazungumzo (Dialogue)
h. Upigwaji wa Picha (Shots)
i. Uigizaji / Vitendo (Actions)
j. Uhamaji (Transition)
k. Usisimuaji (Suspense)

**Ufafanuzi**

**Mazungumzo**

Ni kwa jinsi gani mazungumzo baina ya wahusika yanaendana na mawazo yao, hisia na ushawishi, na yameweza kuonyesha uhusiano baina ya wahusika na kuwakilisha mtazamo wa uhalisia ndani ya mswada

**Mpangilio**
Ni kwa jinsi gani mwandishi amepangilia matukio makubwa ndani ya mswada, hasa kunapokuwa na matendo makubwa, pia na muda uliotumika kuruhusu matukio hayo

**migogoro**
Ni kwa kiasi gani mwandishi amefanikiwa kutengeneza migogoro iliozalisha Maigizo, iliyotengeneza vikwazo,hisia na ushawishi kiasi cha kuteka akili za hadhira , pia migogoro iliyopangiliwa vizuri na kuleta uhalisia

**Wahusika**
Ni jinsi gani wahusika wameshabiina na matukio na vikwazo ndani ya hadithi, na kiasi walichofanikiwa kuendesha matukio kupitia hisia zao,matendo Yao na utashi wao kiasi cha Kufanya hadhira ahisi Kama wao hata Kama matukio hayo sio ya kweli

## 17. KAMPUNI BORA YA UZALISHAJI FILAMU ZA KISWAHILI
Swahili Film Best Production Company

Kampuni bora ya uzalishaji Filamu za Kiswahili itaangaliwa vitu vifuatavyo:-

a. Ubora wa Filamu walizotengeneza kwa mwaka husika

## 18. TUZO YA MAISHA YAMAFANIKIO
Life Time Achievement Award

Tuzo ya maisha ya mafaniko itapendekezwa na kamati ya maandalizi kwa kuangalia vigezo vifuatavyo:-

a. Ushiriki wa muhusika katika utengenezaji na ukuzaji wa filamu za Kiswahili Duniani
b. Awe mfano wa kuigwa na kizazi kipya cha Fiamu za Kiswahili.
c. Awe mtumiaji mzuri wa Lugha ya Kiswahili katika Filamu zake